



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MPWAPWA**



tafadhali taja:

Kumb.Na .HW/MPW/S.10/8B /71

19/04/2022

NAFASI YA KAZI

**MWENYEKITI WA BODI YA AJIRA YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MPWAPWA
KWA KIPINDI CHA MWAKA 2022 HADI 2025**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa anawatangazia Wananchi wote kuwa kuna nafasi wazi ya Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira ya Halmashauri ya Wilaya Mpwapwa kwa kipindi cha Mwaka 2021/2022 - 2023/2024.

SIFA ZA MWOMBAJI

- a) Awe Raia wa Tanzania, Mstaafu katika Utumishi wa Umma mwenye Umri kati ya Miaka 55-65
- b) Awe mwadilifu.
- c) Awe amestaafu katika kada mojawapo ya fani zifuatazo:-
 - Menejimenti ya Rasilimali watu (Human Resource Management).
 - Utawala wa Umma (Public Administration).
 - Sheria (Law).
 - Maendeleo ya Jamii
 - Na Fani zingine zinazoendana na masuala ya Jamii
- d) Pia kazi ya Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira haina mshahara bali Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira atalipwa posho za vikao vya Bodi ya Ajira kadiri vitakapojitokeza au kadiri atakavyohudhuria kwa kuzingatia viwango vya Serikali.

MAELEKEZO

1. Waombaji wote watume barua ya maombi zikiwa na viambatisho vifuatavyo:-
 - a) Cheti cha kuzaliwa
 - b) Vivuli vya vyeti vya masomo na Taaluma (Certified)
 - c) Barua ya utambulisho toka kwa Mwenyekiti wa Serikali za Mitaa ikiwa na picha ndogo ya hivi karibuni.
 - d) Wasifu binafsi (CV).
2. Barua toka kwa wadhamini wawili (2) zikiwa na anuani kamili.
3. Mwisho wa kupokea maombi ya kazi ni tarehe 02/05/2022 saa 9.30 Alasiri.
4. Maombi yote yatumwe **kupitia posta** kwa:-

**Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa,
S.L.P 12,
MPWAPWA**

Mwanahamisi H. Ally

**MWANAHAMISI H. ALLY
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
MPWAPWA**

